

AŞAŞI YA TUNAWEZA

Ilianzishwa na kusajiliwa mwaka 2009 na watu 12 wenye nia ya kuinua na kuboresha maisha ya watu wenye ulemavu.



MALENGO YETU:

- Kuwapatia vijana wenye ulemavu elimu ya ujuzi wa maisha na ufundi ili waweze kujitegemea na kujipatia kipato
- Kuwaandaa na kuwawezesha vijana wenye ulemavu kupata na kuendelea na kazi katika soko la ajira au kujijiri wao wenyewe baada ya kupata ujuzi
- Kuanzisha na kuendesha kituo cha kazi ambacho kinawapatia mazingira bora vijana wenye ulemavu
- Kutetea haki za watu wenye ulemavu

KUWA MMOJA WETU KWA:

- Kumpa mtoto wako mwenye ulemavu nafasi ya kujifunza
- Kuwapatia wengine habari juu ya huduma tuzitoazo
- Kuwashawishi wengine kubadili mtizamo juu ya ulemavu
- Kutusaidia michango ya hali na mali ili tuweze kuwahudumia walengwa wengi zaidi kupitia:

CRDB Nyanza Branch/ Mwanza
A/C no: 01J 101 67 90 800



WASILIANA NASI:

+255-783-386879

+255-784-379877

barua pepe:

tunaweza.mza@gmail.com

www.tunaweza.net

TUNAWEZA



KITUO CHA SHUGHULI NA

MŞAADA WA AJIRA

KWA VIJANA WENYE ULEMAYU



PASIANŞI-ILEMELA
P.O.BOX 10263, PAMBA ROAD
MWANZA - TANZANIA

WALENGWA WETU:



Tunawafundisha vijana wa dini na jinsia zote wenye ulemavu waliofikia umri wa miaka 14 na kuendelea. Kipaumbele zaidi ni vijana

waliomaliza elimu ya msingi katika vitengo vya elimu maalum vilivyo katika jiji la Mwanza na maeneo ya jirani.

HODOMA ZETU:

Tunafundisha ujuzi wa maisha na ufundi kwa kipindi cha miaka miwili.

Tunafungua kituo saa mbili asubuhi hadi saa kumi jioni, Jumatatu mpaka Jumatano.

Tunawasaidia vijana kupata nafasi za kazi kulingana na uwezo na ulemavu wao.

Tunatoa ushauri kwa familia za watoto na vijana wenye ulemavu juu ya upatikanaji wa hudumu mahali tofauti.

Tunatoa semina kwa wazazi/walezi na



asasi juu ya kuboresha maisha ya vijana wenye ulemavu ikiwa ni pamoja na mafunzo ya lugha ya alama.

KAZI ZETU ZA KILA SIKU:

Vijana hujipatia maarifa ya kazi kupitia miradi tofauti.

BUSTANI:

Vijana hushiriki kazi za kuanzisha na kutunza

bustani za mbogamboga, matunda na maua. Pia wanajifunza kutunza mazingira na vifaa na kutengeneza dawa kutokana na mimea ya asili.



UPISHI NA USAFI:

Jikoni vijana hupika vyakula vya kiasili na vya kigeni. Wanajifunza usalama wa vyakula na matumizi sahihi ya vifaa vya jikoni.

USHONAJI NA UPIKAJI WA BATIKI:

Katika miradi hii vijana wanaelekezwa jinsi ya kutumia cherehani, kutengeza batiki kwa kutumia njia tofauti na kuzalisha bidhaa rahisi ili kujiletea kipato baadaye.



ELIMU YA UJUZI WA MAISHA:

Wanafunzi wetu hujifunza juu ya afya, mawasiliano na wanajamii, mambo yanayohusu thamani ya vitu na utu pamoja na utamaduni. Zaidi ya hayo hufundishwa namna ya kuanzisha na kuendesha biashara ndogo ndogo.



USHIRIKIANO NA WAZAZI:

Wazazi hukutana kila baada ya miezi miwili kujadiliana juu ya maendeleo ya vijana wao kituoni.

Wazazi hushiriki kazi kituoni kulingana na mahitaji ili kujijengea uwezo kwa manufaa ya baadaye ya watoto wao.

Wazazi huchangia gharama kidogo kwa ajili ya chakula.

